

# SPACE SCOOP

Bringing news from across the Universe to kids all around the world



EU UNIVERSE  
AWARENESS

## Utaonekana Vipi Kijana Wakati Sio



Kuna baadhi ya watu ambao huwa na muonekano mzuri hata wakiwa na miaka 90, wakati wengine huonekana wazee wakiwa na miaka 50. Hakuna uhusiano wa watu wanavyozeeka na miaka waliyokwisha ishi, ila jinsi wanavyoishi hauthiri kwa kiasi kikubwa. Kuvuta sigara, kunywa pombe na kula vyakula visivyoofaa vinaweza kukufanya uonekane mzee zaidi na kuishi maisha mafupi. Kitu ambacho ni kweli hata kwa makundi ya nyota!

Kundi la nyota kama hili lililopo katika picha, ni kundi la nyota zilizosongamana sana kutokana na nguvu ya uvutano. Zimetengenezwa haraka sana, hivyo nyota hizi zilizaliwa karibu karibu sana. Nyota zilizopo katika picha hii ni baadhi ya nyota za zamani sana katika ulimwengu mzima. Zilitengenezwa katika miaka karibuni bilioni 13 iliyopita na ulimwengu wenye una miaka bilioni 18.7! Ambapo wanaastronomia wamegundua kitu cha ajabu sana kilicho jificha katika moyo wa nyota hizi kubwa na nzee: nyota chang'a!

Ambapo wamegundua kuwa nyota hizi chang'a pia ni za zamani sana. Zimekuwa na bahati ya kuchomwa sindano na kuwa vijana kwa mara ya pili. Pale ambapo nyota mbili nzee zinapogongana na kutengeneza nyota mpya, maada huamishwa. Nyota moja inapata nishati zaidi toka kwa nyjingine. Nyota hiyo huwa nzito, na nyota nzito huvutwa kuelekea katikati ya kundi la nyota. Nishati mpya iliyopata hufanya nyota hizi kung'aa zaidi na kuzifanya zionekane hazina mda mrefu. Siri imefichuliwa!

### COOL FACT

Makundi haya ya nyota zilizosongamana yalikuwa yakinawala galaxi yetu, wakati ule ilipotengenezwa na kulikuwa na maelfu ya makundi haya yanayozurura angani. Leo hii kuna karibu makundi 150 yaliyobakia! Hivyo ni bahati kwa baadhi ya makundi haya kupata maisha mapya.



More information about EU-UNAWE  
Space Scoop: [www.eu-unawe.org/kids/](http://www.eu-unawe.org/kids/)